# Mtandao wa Kuzuia Ukatili wa Kijinsia Siku 16 za Kampeni: **Tamko la vyombo vya Habari**

## **Tumia sauti yako! Chukua hatua Sasa!** Wanaharakati katika kanda wanatoa wito kwa viongozi Kukomesha Ukatili Dhidi ya Wanawake

Kuanzia Novemba 25 hadi Desemba 10 mamia ya asasi za wanaharakati katika eneo la Pembe ya Mashariki na Kusini mwa Afrika wata hamasisha jamii zao na kutoa changamoto kwa viongozi katika ngazi zote kukomesha Ukatili Dhidi ya Wanawake na Wasichana. Mwaka huu siku 16 za Harakati za kampeni kikanda: Paza Sauti, Chukua Hatua, Sasa! Ongoza njia ya kukomesha Ukatili Dhidi Wanawake, madai na kuwasihi viongozi wetu kuongoza mabadiliko kwa kutumia sauti zao kuzungumza, na kushawishi uwezo wao wa kuchukua hatua za kukomesha Ukatili Dhidi ya Wanawake na Wasichana sasa!

Ukatili Dhidi ya Wanawake bado ni changamoto katika kanda na unazuia maendeleo ya kijamii na kiuchumi, unazuia ushiriki sawa wa wasichana na wanawake katika ngazi ya kijamii na kisiasa, una gharama kubwa sana kwa familia, jamii na taifa, na ni ishara kubwa ya kutokuwepo na usawa wa kijinsia na ni ukiukwaji wa haki. Zaidi ya hayo, suala linaloathiri afya ya jamii; Shirika la Afya Duniani lilitoa taarifa kwamba 1 kati ya wanawake 3 wamefanyiwa ukatili wa kimwili na / au kingono katika maisha yao.

**(Tafadhali jaza maelezo na takwimu za gharama za kiuchumi za ukatili, kama zipo, na idadi ya wanawake wanaofanyiwa ukatili katika nchi yako)**

Mashirika mbalimbali, vyombo vya habari, na wanajamii watashiriki katika matukio mbalimbali katika eneo la Pembezoni mwa , Mashariki na Kusini mwa Afrika. Watawaomba viongozi wao kutambua Ukatili Dhidi ya Wanawake kama ukiukwaji wa haki za binadamu na kikwazo kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Sheria na sera nyingi zimewekwa katika kanda, hata hivyo hazitekelezwi kamilifu. Zaidi ya wanachama 800 wa mtandao wa kuzuia ukatili wa kijinsia wanatoa wito kwa hatua madhubuti. Haya ni Madai yetu kwa viongozi:

- Kusema hadharani na kulaani Ukatili Dhidi ya Wanawake.
- Kuendeleza au kuimarisha mpango mkakati ya kitaifa unaojumuisha sekta mbalimbali kurekebisha afya, ustawi wa jamii, polisi, mahakama, elimu na jinsia. Mpango unatakiwa kujumuisha hatua maalumu za uendeshaji wa malengo yanayopimika kwa kila sekta
- Anzisha mfumo wa uratibu kitaifa wenye mamlaka ya kutosha na bajeti kuendeleza, kutekeleza na kufuatilia hatua za kushughulikia Ukatili Dhidi ya Wanawake.
- Hakikisha rasilimali za kutosha zinapatikana kusaidia utekelezaji wa mpango mkakati wa Taifa kwa ajili ya kuzuia na kukabiliana na Ukatili Dhidi ya Wanawake

**(Tafadhali tumia taarifa ulizokusanya wakati ulipokamilisha karatasi kazi ndani ya kifurushi cha kuchukua hatua na utetezi, kurekebisha mahitaji haya ya utetezi na kuyafanya yahusiane na kampeni yako)**



GBV PREVENTION NETWORK
Building Momentum • Fostering Activism

Viongozi katika ngazi mbalimbali wameonyesha dhamira ya kukomesha Ukatili Dhidi ya Wanawake. Wakati wa mkutano wa 25 wa Umoja wa wakuu wa nchi za Afrika ulikua na dhamira ya serikali katika mipango mbalimbali yenye lengo la kuwajengea uwezo wanawake. Mwaka 2015 ni hatua ya nusu ya muongo kwa wanawake wa Afrika ambao unasisitiza maendeleo ya wanawake na kuwajengea uwezo, kwa lengo maalum juu ya amani, usalama na Ukatili Dhidi ya Wanawake. Hizi na ahadi nyingine nyingi zimefanywa na viongozi wetu katika usawa wa kijinsia na kukomesha Ukatili Dhidi ya Wanawake na Wasichana. Ahadi zimesababisha kuwepo na sheria mbalimbali, sera na mipango katika kanda. Huu ni wakati wa kuhakikisha sera na ahadi zilizotolewa kufanya kazi kwaajili ya kusaidia wanawake! Wanachama wa mtandao wa kuzuia ukatili wa kijinsia wanatoa wito kwa viongozi kuonyesha uwajibikaji wao kwa kuchukua hatua zinazotekelezeka ili kukomesha Ukatili Dhidi ya Wanawake na Wasichana.

Kuanzia Novemba 25 (Siku ya Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake) mpaka Desemba 10 (siku ya haki za binadamu), asasi za wanaharakati katika kanda zitachukua kampeni kutoka mitaani kwenye ofisi za viongozi wetu kudai hatua ziweze kuchukuliwa. Watawafikia viongozi wa kisiasa na kiufundi, baraza la mawaziri, wabunge, wakuu wa nchi, viongozi wa kidini na kimila pamoja ili ngazi zote za uongozi wawajibishwe kwa ajili ya kukomesha Ukatili Dhidi ya Wanawake.

Jiunge na harakati! Waombe viongozi wenu waonyesha uwajibikaji wao na kuchukua hatua ya kukomesha Ukatili Dhidi ya Wanawake. Wasiliana na asasi zifuatazo ili kujua jinsi gani unaweza kujiunga na jamii yako kudai uwajibikaji kutoka kwa viongozi wako.

**Jaza maelezo yako hapa:**
**Jina la asasi yako :**
**Mtu wa kuwasiliana:**
**Namba ya simu:**
**Barua pepe:**

Tumia sauti yako, chukua hatua - sasa!

-MWISHO-



GBV PREVENTION NETWORK
Building Momentum•Fostering Activism